

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MADINI**

Telegrams "MADINI".  
Simu: +255 26 2320051  
Nukushi: +255 26 2322282  
Barua pepe: [ps@madini.go.tz](mailto:ps@madini.go.tz)



Barabara ya Kikuyu,  
S.L.P. 422,  
**40474 DODOMA**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UFAFANUZI KUHUSU MAGARI ZAIDI YA 100  
YANAYOSAFIRISHA MAKAA YA MAWE KWENDA NJE  
YA NCHI KUKWAMA ZAIDI YA WIKI MBILI, DODOMA**

Jana tarehe 26 Machi, 2018, katika Taarifa ya Habari ya saa 2 usiku, miongoni mwa habari zilizotolewa kupitia Televisheni ya STAR TV ilieleza kuwa, zaidi ya magari 100 yanayosafirisha makaa ya mawe kutoka mgodi wa TANCOAL NGAKA Wilayani Mbinga kwenda Nchi za Kenya, Rwanda na Uganda yamekwama Mkoani Dodoma kwa zaidi ya wiki mbili yakingoja vibali vya kusafirisha madini hayo nje ya nchi kutoka kwa Kamishna wa Madini. Taarifa hiyo ilitolewa na Kaimu Meneja wa mgodi wa Tan Coal Bw. Edward Mwanga wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini Songea.

**Wizara inapenda kufafanua kuwa**, katika kipindi cha wiki mbili zilizopita Wizara imepokea jumla ya maombi ya vibali **69** hadi tarehe 26 **Machi, 2018** ya Kampuni hiyo kwenda nchi za Nje kwa mchanganuo ufuatao;

<b>No</b>	<b>TAREHE/KUPOKEA VIBALI</b>	<b>JUMLA YA MAOMBI</b>	<b>TAREHE/KUSAINIWA VIBALI</b>
1.	12 Machi, 2018	07	13 Machi, 2018
2	14 Machi, 2018	12	16 Machi, 2018
3	16 Machi, 2018	06	19 Machi, 2018
4	19 Machi, 2018	13	20 Machi, 2018
5	20 Machi, 2018	01	20 Machi, 2018
6	21 Machi, 2018	03	22 Machi, 2018
7	23 Machi, 2018	10	23 Machi, 2018
8	26 Machi, 2018	17	27 Machi, 2018
<b>JUMLA</b>		<b>69</b>	

Aidha, baada ya mapitio ya vibali vilivyotolewa kwa Kampuni ya TanCoal katika kipindi cha wiki mbili zilizopita Wizara imejiridhisha kuwa hakuna kibali kilichochukua zaidi ya siku **2** kutolewa.

Kwa mujibu wa Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, vibali vya kusafirisha madini kwenda nchi za nje vinatolewa na Tume ya Madini kupitia kwa Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini. Aidha, hivi sasa kuna Kaimu Mtendaji Mkuu wa Tume ya Madini ambaye anahusika kutoa vibali hivyo.

Hata Hivyo, Wizara inaendelea kuchukua hatua za kuboresha utaratibu wa utoaji wa vibali ili vitolewe ndani ya muda mfupi zaidi.

**Imetolewa na;**

Prof. Simon Msanjila  
**KATIBU MKUU**  
**27 Machi, 2018**